JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALAZAMIKOANASERIKALIZAMITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

SHULE YA SEKONDARI KILI

# MAELEKEZOYAKUJIUNGANAKIDATOCHATANOKATIKA SHULE YA SEKONDARI KILI MWAKA.........

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU –TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA VIJIJINI**

**Shule ya Sekondari Kili**
**S.L.P.4**

**Bukene**

**Tarehe:…………..**

**Mzazi/MleziwaMwanafunzi………**

**S.L. P……………...**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KILi HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA DC MKOA WA TABORAMWAKA………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule yetu mwaka……………na atasoma tahasusi ya HGK/HGL/HGLi/ HGFa. Shule ya Sekondari KILi ipo umbali wa Kilometa 40 kutoka Nzega mjini.Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Nzega mjini Nauli ni Shilingi 5000 kwa basi na kutoka kituo cha Bukene hadi shuleni ni kilomita 2.5, nauli ni shilingi 2000 kwa pikipiki. Muhula wa Masomo utaanza tarehe kwa tangazo la Serikali.

**Mambomuhimuyakuzingatia:-**

**Sare za Shule**

a) Shati mbili nyeupe mikono mirefu(aje nazo na zitakaguliwa).

b) Viatu pea mbili vyeusi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba. (c)

Soksi nyeupe ndefu pea mbili.

c) Sketi damu ya mzee mbili zenye rinda box kubwa mbele moja na nyuma moja, rinda ndogondogo kulia 2 na kushoto 2, sketi ziwe ndefu hadi kufika chini kabisa (ziguse kisigino) Kama inavyoonekana kwenye picha.Kinyume na hivyo zitakataliwa.

d) Sweta rangi damu ya mzee mbili mshono alama ya "V" shingoni.

e) Tai mbili ndefu rangi damu ya mzee.

f) Hijabu mbili rangi nyeupe (isiwemtandio)Kama inavyoonekana kwenye picha.

g) Sketi nyeusi mbili zenye rinda box kubwa mbele moja na nyuma moja,rinda ndogondogo kulia 2 na kushoto 2, sketi ziwe ndefu hadi kufika chini kabisa (ziguse kisigino)

h) Tisheti mbili rangi ya damu ya mzee yenye kola nyeupe ya kushindia (Kama utapenda itapatikana Shuleni kwaTsh.13,000/=kila moja)

NB: Aje amevaa sare sketi nyeusi,shati nyeupe na tai







**Nguo za Michezo:**

A. Tracksuit moja rangi ya blue bahari

B. Raba pea moja ya kufunga na kamba

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 8 (Kaunta).
ii. Aje na kopi ya cheti cha kuzaliwa
iii. Aje na **Bima ya Afya**
iv. Ream mbili za Karatasi "A4" kwa kila mwaka
v. Vitabu vya masomo yatahasusi husika ya mwanafunzi;
vi. Calculator;
vii. Godoro la sponji futi2½ kwa 6.
viii. Mashuka pea 2 rangi bluu bahari, blanket1,foronya ya godoro1, chandarua 1 futi 3½ kwa sita;
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Kwanja 1 (HGK/HGL/HGLi/HGFa), jembe1 na mpini wake (HGK/HGL/HGLi/ HGFa), mopa (HGK), mfagio 1 wa ndani (HGL)na wanje (HGLi na HGFa).
xi. Vyombo vya chakula:Sahani moja ya bati ya vyumba(Compartment Plate) ,Kijiko, Kikombe cha bati 1,Ndoo za plastiki 2 zenye mifuniko.



*Sahani ya bati ya vyumba (Compartment Plate)*

**Michangombalimbali**

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| | MchangowaUendeshajiwaShule | **65,000/=** |
| | Tahadhari | **5000/=** |
| | Nembo | **5000/=** |
| | KitambulishochaShule | **5000/=** |
| | **Jumla** | **80,000/** |

**2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

ShuleinaendeshwakwamujibuwaSheriayaElimuNa.25yamwaka l 978na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. l0 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo nl pamo a na;

**SherianaKanunizaShule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Night Preparations) naAlfajiri(Moming
i. Preparations)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule atakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi. Pia, kipindi chote mwanafunzi awapo shuleni hataruhusiwa kuongea na mzazi/mlezi wake moja kwa moja kupitia simu yoyote ile bali mawasiliano baina ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yatafanyika kupitia mwalimu wa mawasiliano/wa darasa wa mwanafunzi husika. Namba za mwalimu wa mawasiliano zitatolewa na mkuu wa shule pindi mwanafunzi atakaporipoti.
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwana kitandaalichopangiwa.Nimarufukumwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalohakupangiwa.Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwa (Msiba au Ugonjwa).
- Mwanafunzi kamwe haruhusiwi kuja na nguo za kawaida(za nyumbani).
- Haturuhusu kusuka kwa mwanafunzi yeyote.

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuriamasomokwazaidiyasiku90bilataarifa/utoro;
iii. Kugomanakuhamasishamgomo;
iv. Kutoalughachafukwawanafunziwenzake,walimu/walezinajamiikwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KILi.**

**Saini ya Mkuu wa Shul**----------------**Jina la Mkuu wa Shule: ESTON KATIRIGE**

**Mhuri wa Mkuu wa Shul**est'IJLE..YA.SEKONDAR... LA....

MKUU WA SHULE
S. L. P. 4
8UKENE

6

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).

Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husikaambaye ni mwanafunzi ni mgojwa nayukomahututihivyomzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

1. Mkuuwashule:0787295714/0769590997
2. MakamuMkuuwaShule:0782785288
3. MwandamiziTaaluma:0762623897
4. MwandamiziMalezi:0755 716 899

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURIYA WILAYA YA NZEGA**
**SHULE YA SEKONDARI KILi**

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government Medical Officer and returned to the Head master Kill Secondary School)

NA.ME .

(Please examine the student named above and comment on his/her hearth recording to the following items. Kindly put a tick in out of either TES or NO whichever is applicable)

I. Does the student have problem in connection with

A. Sight? — I. NO .
IF YES State — 2. YES .

B. Hearing? — 1. NO .
IF YES State — 2. YES .

C. TB — 1. NO .
IF YES State — 2. YES .

D. Blood pressure — 1. NO .
IF YES State — 2. YES .

E. Any other health problems — 1. NO .
IF YES State — 2. YES .

F. Syphilis and other veneral diseases — 1. NO .
IF YES State — 2. YES .

L. No please State .

Name and signature — Designation .

……..……..………… Date — Official stamp

**SHULE YA SEKONDARI KILi**
**S.L.P 04 BUKENE**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

i. Jina la mwanafunzi……………………………………………………………………..
ii. Jina la baba………………………………………………………………..................
iii. Jina la mama ……………………………………………………….................
iv. Jina kamili la mlezi…………………………………………………...................
v. Anuani ya mzazi/mlezi……………………………………………..........................
vi. Uhusiano wa mlezi ……………………………………………...........................
vii. Kazi ya baba.(mkulima,mfanyabiashara,mfanyakazin.k)…………………………….
viii. Kama ni mkulima,zao muhimu analolitegemea ni……………………………………
ix. Kama nimfanyabiashara,biasharayake ni ………………………………………
x. Kama nimfanyakazi,kazi yake ni ………………………………………………
xi. Afya ya mwanafunzi,kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi…………………………………………………….......................................
……………………………………………………………………………………………………
… ………………………………………………………………………….............................................
xii. Madhehebu ya dini ……………………………………………….............................................
xiii. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi

jina kamili | kazi yake | namba ya simu

1 ……………………………… ………………………..…………………………. Bandika picha

2 ……………………………… ………………………..…………………………. Bandika picha

3 ………………………………..………………………………………………………. Bandika picha

4 ………………………………..………………………………………………………. Bandika picha

**HALMASHAURIYA WILAYA YANZEGA**

**SHULEYA SEKONDARI KILi**

**S.L.P 04 BUKENE**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Jina la mwanafunzi ……………………………………….

Jina la mzazi/mlezi ………………………………………….

Anuani ya mzazi/mlezi ……………………………………….

Uhusiano............................(Mfano;baba,mjomba,kaka,dada n.k)

Mimi........................................................................... nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zangu zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa **ili** kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA mu KABISA NA KUTII viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwanjia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi………………………………….tarehe ……………………......................

Mimi …………………………… Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………….. .

ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi …………………………… tarehe …………………………....................